

illustrert av
ALYONA POTYOMKINA

OSLOMET

NAFO

Nasjonalt senter for flerkulturell oppl ring



MBOGA KUBWA YA MAJANI TURNIPU



IVAN
FRANKO

1856 - 1916

Hii hadithi inajulikana maeneo mengi duniani. Toleo la NAFO la Mboga kubwa ya majani ya turnipu imehamasishwa na toleo la hadithi Рипка (Ripka) ya mwaka 1891 ya mwandishi kutoka Ukraine Ivar Frankos. Toleo lake lina sifa ya majina ya kuchekesha ya wahusika na marudio kama mbinu ya kusimulia hadithi. Ivan Franko aliandika hadithi na mashairi kwa watoto, pia mashairi na hadithi ndefu za kubuniwa (riwaya) kwa watu wazima. Mji wa Ukraine wa Ivano-Frankivsk unaitwa hivyo, kwa sababu ya jina lake.

Denne fortellingen er kjent mange steder i verden. NAFOs versjon av *Den gigantiske nepen* er inspirert av den ukrainske forfatteren Ivan Frankos versjon av eventyret Рипка (Ripka) fra 1891. Hans versjon kjennetegnes av de artige navnene på karakterene og gjentakelse som fortellerteknikk. Ivan Franko skrev eventyr og dikt for barn, og også dikt og romaner for voksne. Den ukrainske byen Ivano-Frankivsk er oppkalt etter ham.

Hapo zamani za kale kulikuwa na familia iliyokuwa inaishi katika shamba lililokuwepo katika kijiji kidogo. Katika shamba hilo aliishi babu aliyekuwa anaitwa Androshka, bibi aliyekuwa anaitwa Maroshka, mjukuu wao aliekuwa anaitwa Minka, mbwa aliyekuwa anaitwa Finka, paka aliekuwa anaitwa Varvarka na panya aliekuwa anaitwa Siromanka.

Det var en gang en familie som bodde på en gård i en liten landsby. På gården bodde bestefar Androshka, bestemor Maroshka, barnebarnet Minka, hunden Finka, katten Varvarka og musen Siromanka.



Ilipokuwa kipindi cha msimu wa mvua nyingi (masika) babu Androshka alienda kwenye bustani. Alikuwa amebeba koleo aina ya jembe , akachimba shimo katika udongo na kupanda mbegu ya mboga ya majani turnipu.

Akawa anaimwagilia maji ile mbegu ndogo kila siku, na baada ya muda iliota kwa kuchipua mmea mdogo kutoka ardhini.

Da det ble vår, gikk bestefar Androshka ut i hagen. Han tok med seg en spade, gravde et hull i jorden og plantet et lite nepefrø.

Han vannet det lille frøet hver eneste dag, og etter en stund vokste en liten spire opp av bakken.



Mmea uliota ukawa mboga ya majani ya turnipu iliyokuwa inakuwa kubwa kila siku inayopita.

Siku ya kwanza ilikuwa ndogo kama panya.

Siku ya pili ikawa kubwa kama kukunja ngumi ya mkono.

Siku ya tatu ikawa kubwa kama kiazzi chekundu au beetroot ni mmea wa mviringo mwekundu kama kiazzi na kina mizizi).

Siku ya nne ukawa mkubwa sawa na vaizi vyekundu viwili (rødbete kwa kinorwei).

Siku ya tano, Babu alipoenda kuona mboga ya majani turnipu, ilikuwa kubwa kama kichwa chake.

Spiren ble til en nepe som vokste seg større for hver dag som gikk.

Den første dagen var den like liten som en mus.

Den andre dagen hadde den blitt like stor som en knyttneve.

Den tredje dagen hadde den blitt like stor som en rødbete.

Den fjerde dagen hadde den blitt like stor som to rødbeter.

Da bestefar gikk ut for å se på nepen den femte dagen, var den like stor som hodet hans!



Babu Androshka alikuwa amefurahi na kuridhika, alikuwa anafurahia kuwa ataivuta kwa kuingóa mboga ya majani ya turnipu, kutoka kwenye udongo au aridhini.

Akashika majani ya mboga ya majani ya turnipu, akaiweka miguu yake vizuri aridhini na kuvuta kwa nguvu na uwezo wake wote. Alivuta na kuhangaika siku nzima lakini ile mboga ya majani kubwa ya turnipu ilishindwa kutoka aridhini.

Babu Androshka alimuita bibi kwa kupiga kelele, “Maroshka!!

“njoo unisaidie kuvuta na kungóa!”

Bestefar Androshka var veldig fornøyd, og gledet seg til å dra nepen opp av jorden.

Han tok tak i bladene på nepen, satte føttene sine godt ned i bakken og dro alt han kunne. Han dro og slet hele dagen lang, men den gigantiske nepen satt bom fast i bakken.

Bestefar Androshka ropte på bestemor Maroshka:

«Kom og hjelp meg med å dra!»



Bibi alikuja kwa haraka iwezekanavyo. Babu Androshka alikuwa ameshika mboga ya majani ya turnipu na bibi Maroshka akashika shati la babu, na wote wakavuta kwa nguvu kwa uwezo wao na nguvu zao zote. Walivuta na kuvuta kwa uwezo wao wote lakini ile mboga ya majani ya turnipu kubwa ilishindwa kutoka aridhini.

Bibi Maroshka akamuita mjukuu wake kwa kupiga kelele “Minka!!

“Njoo utusaidie kuvuta na kungóa!”

Bestemor kom så fort hun kunne. Bestefar Androshka tok tak i nepen og bestemor Maroshka tok tak i bestefars skjorte, og så dro de alt de kunne. De dro og dro, men den gigantiske nepen satt fortsatt bom fast i bakken.

Bestemor Maroshka ropte på barnebarnet sitt, Minka:

«Kom og hjelp oss med å dra!»



Mjukuu Minka alikuja akiruka ruka. Babu Androshka alikuwa ameshika mboga ya majani ya turnipu, bibi Maroshka alikuwa ameshika shati la babu na mjukuu Minka akashika mkanda wa bibi, na wote wakavuta kwa nguvu zao zote na uwezo wao wote . Walivuta na kuvuta kwa nguvu zao zote na uwezo wao, lakini ile mboga ya majani ya turnipu kubwa ilishindwa kutoka aridhini.

Mjukuu Minka akamuita mbwa wake aitwae Finka kwa kupiga kelele,”Finka!

“njoo utusaidie kuvuta na kungóa!”

Barnebarnet Minka kom hoppende. Bestefar Androshka tok tak i nepen, bestemor Maroshka tok tak i bestefars skjorte og barnebarnet Minka tok tak i beltet til bestemor, og så dro de alt de kunne. De dro og dro, men den gigantiske nepen satt fortsatt bom fast i bakken.

Barnebarnet Minka ropte på hunden sin, Finka:

«Kom og hjelp oss med å dra!»



Mbwa Finka alikuja akikimbia. Babu Androshka alikuwa ameshika mboga ya majani ya turnipu, bibi Maroshka alikuwa ameshika shati la babu, mjukuu Minka ameshikilia mkanda wa bibi, na mbwa Finka ameshikilia sketi ya mjukuu. Walivuta na kuvuta lakini ile mboga kubwa ya majani ya turnipu ilishindwa kutoka aridhini.

Mbwa Finka akamuita rafiki yake, paka Varvarka kwa kupiga kelele, “Varvarka!

“njoo utusaidie kuvuta na kungóa!”

Hunden Finka kom løpende. Bestefar Androshka tok tak i nepen, bestemor Maroshka tok tak i bestefars skjorte, barnebarnet Minka tok tak i beltet til bestemor og hunden Finka tok tak i skjørtet til barnebarnet. De dro og dro, men den gigantiske nepen satt fortsatt bom fast i bakken.

Hunden Finka ropte på venninnen sin, katten Varvarka:

«Kom og hjelp oss med å dra!»



Paka Varvarka alikuja kwa kutembea taratibu, polepole na kwa uangalifu kwa kunyata. Babu Androshka alikuwa ameshika mboga ya majani ya turnipu, bibi Maroshka alikuwa ameshika shati la babu, mjukuu Minka ameshikilia mkanda wa bibi, mbwa Finka ameshikilia sketi ya mjukuu na paka Varvarka ameshikilia mkia wa mbwa. Walivuta na kuvuta lakini ile mboga kubwa ya majani ya turnipu ilishindwa kutoka aridhini.

Paka Varvarka akamuita mnyama kipenzi chake, panya Siromanka:

“njoo utusaidie kuvuta na kungóa!”

Katten Varvarka kom luskende. Bestefar Androshka tok tak i nepen, bestemor Maroshka tok tak i bestefars skjorte, barnebarnet Minka tok tak i beltet til bestemor, hunden Finka tok tak i skjørtet til barnebarnet og katten Varvarka tok tak i halen til hunden. De dro og dro, men den gigantiske nepen satt fortsatt bom fast i bakken.

Katten Varvarka ropte på kjæledyret sitt, musen Siromanka:

«Kom og hjelp oss med å dra!»



Panya Siromanka alikuja kwa haraka.

Babu Androshka alikuwa ameshika mboga ya majani ya turnipu, bibi Maroshka alikuwa ameshika shati la babu, mjukuu Minka amemshikilia mkanda wa bibi, mbwa Finka ameshikilia sketi ya mjukuu, paka Varvarka ameshikilia mkia wa mbwa na panya Siromanka amemshikilia paka kwenye mguu. Walivuta kwa nguvu na uwezo wao wote.

Walivuta na kuvuta, na ghafla...

Musen Siromanka kom pilende. Bestefar Androshka tok tak i nepen, bestemor Maroshka tok tak i bestefars skjorte, barnebarnet Minka tok tak i beltet til bestemor, hunden Finka tok tak i skjørtet til barnebarnet, katten Varvarka tok tak i halen til hunden og musen Siromanka tok katten i labben, og så de dro alt de kunne.

De dro og dro, og plutselig ...



BAM! Ile mboga kubwa ya majani ya turnipu ikang'oka na kutoka kwenye udongo.

Mboga ya majani ya turnipu ikamuangukia babu Androshka, ambae alimuangukia bibi Maroshka, ambae alimuangukia mjukuu Minka, ambae alimuangukia mbwa Finka, ambae alimuangukia paka Varvarka wakati panya Siromanka...

BAM! Den gigantiske nepen løsnet fra jorda!

Nepen landet på bestefar Androshka, som falt på bestemor Maroshka, som falt på barnebarnet Minka, som falt på hunden Finka, som falt på katten Varvarka, mens musen Siromanka ...




...chwiish! Anaingia na kupotelea kwenye shimo lake la panya.

... SVISJ! Hun forsvant inn i musehullet sitt.





Denne fortellingen finner du gratis på flere språk på **morsmål.no**. 
Der finner du også flere fortellinger fra hele verden med tilhørende ressurser.